

CultureTalk Tanzania Video Transcripts: <http://langmedia.fivecolleges.edu>
Story of the Hyena and the Hare

Swahili transcript:

Upendo: Na mimi nakumbuka nilipokuwa mdogo, kuna hadithi moja ya sungura na fisi hao hao. Ni kwamba, ile hadithi ilikuwa inafundisha kwamba hutakiwi kuwa na tamaa, ni kwamba inaonekana kwamba fisi alikuwa na tamaa. Kwamba, sungura na fisi walikuwa wamealikwa kwenye sherehe. Na, sasa sherehe zilikuwa...zilikuwa mbili, sehemu mbili tofauti na walikuwa wamealikwa muda huo huo mmoja. Kwa hiyo, sungura yeye aliamua tu aende kwenye sherehe moja, lakini fisi akasema aah! Nataka nikale vyakula sehemu zote mbili, sherehe zote mbili. Kwa hiyo akawa ame-plan aende, aende sherehe ya kwanza, atoke pale akimbie tena aende akale na sherehe ya pili. Sasa unajua nini kilitokea? Alivyoenda sherehe ya kwanza amefika kule amekuta ndio vyakula ndio sasa viko katika hatua ya mwisho; ndio vinaishiaishia kupikwapikwa vizuri, kuwekwawekwa vizuri, kwa hiyo alikuta watu bado hata hawajaanza kula. Kwa hiyo akasema, aah! Kwa vile hapa hawajaanza kula, ngoja nikimbie niwahi ile sherehe nyingine. Nikale kule, nikitoka, nije huku. Basi, akaondoka, akaenda hiyo...hiyo sherehe nyingine ya pili. Anafika kule, ndio anakuta watu wanamalizia...ndio vyombo vinakusanywa, watu wameshakula, wamemaliza. Akaona mm! hapa sasa ngoja niiwahi tu ile ile ya kwanza ili nisije nikakosa. Kakimbia kafika kule, anakuta ndio maharusi hao wanaondoka, watu walishakula wamemaliza.

Happy: (kicheko)

Upendo: Kwa hiyo yaani kutokana na nini ..ile tamaa akawa ama..amekosa kote yaani. Kwamba tamaa ya fisi yaani ikamfanya akose kote. Kwa hiyo huwa tulikuwa tunafundishwa kwamba hutakiwi kuwa na tamaa, unaona eeh? Kwa hiyo ilikuwa inatufundisha hutakiwi uwe na tamaa.

English Translation:

Upendo: The story about the hyena and the hare goes like this: A hare and a hyena were invited to attend a wedding. There were two weddings which took place in two different places at the same time. The hare decided to attend one wedding, but the hyena wanted to attend both weddings so he could eat food from both weddings. So he planned to go and eat at one wedding, and afterwards go to the other wedding. Do you know what happened? When he went to the first wedding, he found that the food was still not ready. So he decided to go to the other wedding, hoping that when he returned, the food would be ready. When he arrived there, he found that the people had just finished eating. Plates were being removed and cleaned. He said to himself, "I'll go back to the first wedding so that I won't miss the food, and by this time, the food will be ready." When he arrived there, he found the bride and groom leaving, and people had finished eating. The wedding was almost over.

Happy: Laughter.

Upendo: Because he wanted to eat at both weddings, he missed both. So we were told that we should not be like a hyena because greed is a bad thing.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.